
**UCHANGANUZI WA MAKOSA YAKISARUFI NA ATHARI ZA KAKATIKA
MATOKEO YA WANAFUNZI WA KISWAHILI CHUONI METROPOLITAN
MAGHARIBI MWA UGANDA**

1 Karuhanga Deusdedit¹, 2 Dr. Beverlyne Asiko Ambuyo

1, 2 Metropolitan International University

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Uganda Jijini Mbarara Suala la utafiti ni kwamba kumekuwa na matokeo mabaya katika mitihani ya wanafunzi wa Kiswahili kulingana na ripoti na rekodi za ofisi ya msajili wa Chuo Kikuu cha kitaifa cha Metropolitan miaka ya 2018 hadi 2021. Kwa hivyo utafiti huu ulifanywa kwa azma ya kubaini athari za makosa ya kisarufi yanayowapelekea wanafunzi wa Kiswahili kupata matokeo mabaya katika mitihani yao. Madhumuni ya utafiti huu ni kutambulisha na kuainisha makosa ya kisarufi yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili na kudhihirisha athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya mitihani ya Kiswahili Chuoni Metropolitan. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi Makosa iliyoanzishwa na (Corder 1969), Maswali yaliyoongoza utafiti huu ni: Je, ni makosa ya aina gani katika mitihani yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan? Je, makosa ya kisarufi yana athari gani kwa matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan? Katika upeo, utafiti huu ulichanganua makosa ya kisarufi na athari zake katika matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan. Kundi lengwa katika utafiti huu ni wanafunzi wanaojufunza Kiswahili Chuoni Metropolitan pamoja na wahadhiri wao. Wanafunzi mia moja na watano na wahadhiri wawili ndio waliteuliwa kuchunguzwa katika utafiti huu ambapo athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi yalibainika. Hojaji na uchunguzi shirikini mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji wa data. Data ya utafiti huu ni makosa ya kisarufi ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Metropolitan Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya Kithamano. Matokeo ya utafiti huu yatachangia pakubwa katika uwanja wa upataji lugha, na kadhalika utawafa wanafunzi umetarajiwa kuwafaa wanafunzi wa Kiswahili

na walimu wao wa lugha, wakuza mitaala ya Kiswahili na watafiti mbalimbali wa lugha.

Usuli wa Mada

Mdee (1986) anaeleza sarufi kama mfumo wa kanuni za lugha zinazoonyesha uwezo wa lugha hiyo. Kulingana na (Mgullu 1999), Sarufi ni dhana inayojumuisha vipengele vya fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia na Semantiki. Pia Tuki (1990), inaeleza sarufi kama dhana inayoeleweka kuwa na jumla ya kanuni zinazoongoza kuongea na kuandika lugha sahihi. Kwa hivyo, kulingana na utafiti huu mtafiti anatumia sarufi kama usahihi wa sentensi na maneno ya Kiswahili. Sentensi sahihi ya kisarufi lazima izingatiwe na upatanishi wa ngeli, vivumishi, virejeshi, vibaini, vitenzi, udogo, na ukubwa nakadharika kulingana na mazingira inayotumika.

Makosa ya kisarufi ni matokeo ambayo msemaji wa lugha hutamkwa au kuyandika maneno bila kufuata sheria zinazotawala lugha, ni pale lugha inapotumika tofauti na malengo hupoteza lengo na madhumuni ya mzungumzaji kwa msikilizaji wake. Kila lugha hutawala matumizi ya lugha ili watu waweze kuelewana. Kanuni hizo huweza kupeleka makosa kujitokeza na kwa hivyo kupotosha ufasaha wa lugha. Makosa ya kisarufi ni pamoja na yale ya kimsamiati na kimatamshi. Athari za makosa ya kisarufi hutokea pale ambapo msemaji wa lugha hutamka au kuandika maneno bila kufuata sheria zinazotawala lugha. Kulingana na ripoti na rekodi za ofisi ya msajili wa Chuo Kikuu cha Metropolitan Magharibi mwa Uganda zinaonyesha kuwa wanafunzi wa Kiswahili wa mwaka 2018 hadi 2020 walipata matokeo mabaya katika mitihani yao. Matokeo ya utafiti huu, yalibaini kwamba wanafunzi wanapoandika insha zao ndiyo yanayowapelekea kuanguka mitihani yao

Makosa mengi ni uteuzi wa msamiati na kwa hivyo kusababisha makosa ya kimuundo wa neno na wa sentensi. Kwa mfano mtu akisema ‘ninapanda mti’ usemi huu unaweza kukanganya mtu asijue ni kupanda kupi anakokusudia. Je! ni kuotesha au ni kukwea mti ikiwa muktadha hautazingatiwa. Na wakati mwingine maana inaweza ikapotea kabisa. Na hii ndiyo kusema uandishi unahitaji ufasaha wa uteuzi wa sarufi.

Mbaabu (2005) anaelezea kuhusu makosa yanayofanywa mara kwa mara na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii. Miongoni mwa makosa yaliyobainika ni yale yanayotokana na athari za lugha ya kwanza kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kwa mfano mnyankore akiwa anatumia kinyankore kama lugha yake ya kwanza mara nyingi anachanganya maneno ya Kiswahili na ya kinyankore, kama neno 'soma' analitumia kuwa "shoma" yaani hilo ni kosa la kisarufi katika Kiswahili sanifu.

Wataalamu wengi katika uchunguzi wao wanaeleza kuwa licha ya athari za kimatamshi, watumiaji wengi huwa rahisi sana kutambua kabila la msemaji kwa sababu ya athari za matamshi kutoka katika lugha mama (lugha yake ya kwanza). Alibaini pia kwamba makosa ya kawaida ambayo hufanywa na watu wazima wanapotumia lugha ya Kiswahili miongoni mwa jamii za Kenya huzua athari za lugha zao za mama kwenye Kiswahili na kwa hivyo hukikosesha ladha na hata pengine kugeuza muundo wake. Kwa mnasaba huo utafiti wake uligusana na huu ambao ulishughulikia athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan.

Utafiti huu ulichunguza athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Uganda Jijini Mbarara. Makosa hayo ya kisarufi na athari zake katika matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili hazijawekwa wazi. Mtafiti amebaini kwamba athari za makosa ya kisarufi yanaweza kudhihirishwa katika uandishi wa insha na imla. Kwa hivyo, mtafiti amebaini kwamba wahadhiri wangukuwa wanawapa hizo kazi za uandishi wa insha na imla na kuzisahihisha basi na makosa yangepungua au kuondoka. Lugha ya kwanza huathiri lugha ya pili kulingana na (Tembena na Norton (2008)). Hali hii ilikuwa haijulikani iwapo lugha mama za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Metropolitan Magharibi mwa Uganda ndizo zinazosababisha matokeo mabaya katika mitihani, mifano ya lugha za kimama ni kama kiganda, kinyankore, Kikiga, Kikonzo na kadhalika, na nyinginezo na mara nyingi lugha hizi zinaathiri Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, utafiti huu ulifanyika kwa nia ya

kuziba pengo hilo la kielimu, kuchanganua makosa, kuainisha makosa ya kisarufi. Kwa hivyo, lengo kuu la kufanya utafiti huu ni kutambua na kuanisha athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan.

Suala la Utafiti

Kumekuwa na matokeo mabaya katika mitihani ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Uganda. Kwa hivyo utafiti huu ulifanywa kwa azma ya kubaini athari za makosa ya kisarufi yanayowapelekea wanafunzi wa Kiswahili kupata matokeo mabaya katika mitihani yao. Kiswahili ni lugha inayofundishwa katika Chuo Kikuu cha Metropolitan Magharibi mwa Uganda kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili

Madhumuni ya Utafiti

1. Kutambulisha na kuainisha makosa ya kisarufi yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Metropolitan Magharibi mwa Uganda.
2. Kudhihirisha athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya mitihani ya Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Uganda.

Maswali ya Utafiti

3. Je, ni makosa ya aina gani katika mitihani yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Uganda?
4. Je, makosa ya kisarufi yana athari gani kwa matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Uganda?

Umuhimu wa Utafiti

Mada hii ya utafiti ilichaguliwa kwa azma ya kuondosha athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi ambao ni watahiniwa wa mitihani ya somo la Kiswahili. Utafiti huu utasaidia tafiti zingine kuhusu uwanja wa kusahihisha athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi. Isitoshe, matokeo ya utafiti huu ni mchango katika uwanja wa upataji lugha na unatarajiwa kuwafaa wanafunzi wa Kiswahili na walimu wao wa lugha, wakuza mitaala ya Kiswahili na watafiti mbalimbali katika uwanja huu wa lugha kama marejeleo ya kazi zao.

Kiunzi cha Nadharia

Mdee na wenzake, (2011), wanaeleza kuwa nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Massamba (2004), kama alivyonukuliwa na Msanjila (2006), anasema kuwa, nadharia ni utaratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumika kama kielelezo cha kuelezea jambo.

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia nadharia ya uchanganuzi makosa (NUM). Kwa vile utafiti huu ulinuia kutambua na kuainisha makosa ya kisarufi yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan. Nadharia ya uchanganuzi Makosa ni muhimu kwa sababu humwezesha mtafiti kutambua na kuainisha makosa ya kisarufi yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili katika mitihani.

Nadharia hii (NUM) ilianzishwa na Corder (1969), na kuendelezwa na Etherton (1977), Narrish (1983) na huchunguza makosa kwa kuzingatia mihimili. Kulingana na mwanaisimu Corder, mtafiti hutumia mihimili ifuatayo katika uchanganuzi makosa:

1. **Kukusanya makosa.** Makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi ilikukusanywa kutoka kwa insha zao na kutokana na shirikishi ya wahadhiri.
2. **Kutambua makosa.** Makosa ya kisarufi yaliweza kutambuliwa kwa kupigiwa mstari.
3. **Kuainisha makosa.** Makosa ya kisarufi huwekwa katika makundi mbalimbali, kwa mfano makosa ya uendelezaji wa maneno ya kisarufi.

4. **Kuhesabu makosa.** Idadi ya makosa ya kisarufi katika kila kundi hutambuliwa.
5. **Kutambulisha vipengele vyenye makosa.** Vipengele vya lugha vinavyotatiza wanafunzi na kusababisha makosa ya kisarufi katika matokeo hubainishwa, kwa mfano fonimu fulani, virejeshi, vitenzi, nyakati (njeo), miundo ya silabi na vishazi tegemezi.
6. **Chanzo cha makosa.** Mambo yanayosababisha makosa ya kisarufi hayo hubainishwa, kwa mfano athari za lugha ya kwa kwanza, hujumlishaji- mno, tafsiri sisizi, na ukosefu wa utaratibu mmoja wa kuendeleza maneno.
7. **Kurekebisha makosa.** Makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi husahihishwa kwa kuonyesha majibu yaliyotarajiwa kwenye karatasi ya insha. Njia zingine za kurekebisha makosa ni pamoja na kuwapa wanafunzi mazoezi ya kutosha wakati wa somo, kutumia vitabu mwafaka kuwafundishia na pia kutumia mbinu za kufundishia.
8. **Kuonyesha athari inayosababishwa na makosahayo.** Baadhi ya athari zinazotokana na makosa ya kisarufi ni pamoja na kutatanisha mawasiliano, kufedheheka, kuanguka mitihani, kukosa kazi na watu kutokuamini

Maelezo ya Istilahi

Sarufi: Mdee (1986) anaeleza sarufi kama mfumo wa kanuni za lugha zinazoonyesha uwezo wa lugha hiyo. Kulingana na (Mgullu 1999), Sarufi ni dhana inayojumuisha vipengele vya fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia na Semantiki. Pia Tuki (1990), inaeleza sarufi kama dhana inayoeleweka kuwa na jumla ya kanuni zinazoongoza kuongea na kuandika lugha sahihi.

Kwa hivyo, kulingana na utafiti huu mtafiti anatumia sarufi kama usahihi wa sentensi na maneno ya Kiswahili. Sentensi sahihi ya kisarufi lazima izingatiwe na upatanishi wa ngeli, vivumishi, virejeshi, vibaini, vitenzi, udogo, na ukubwa nakadharika kulingana na mazingira inayotumika.

Makosa ya Kisarufi. Makosa ya kisarufi ni matokeo ambapo msemaji wa lugha hutamka au kuandika maneno bila kufuata sheria zinazotawala lugha. Lugha inapotumika tofauti na malengo hupoteza lengo na madhumuni ya mzungumzaji kwa

msikilizaji wake. Kila lugha hutawala katika matumizi ya lugha ili watu waweze kuelewana kanuni hizo zinapovunjwa au kikiukwa huweza kusababisha makosa kujitokeleza na upotovu katika lugha. Makosa ya kisarufi yanaweza kugawanyika katika sehemu zifuatazo;

- Makosa ya kimuundo
- Makosa ya kimsamiati
- Makosa ya kimatamshi
- Kuongeza vitamkwa au Viambishikuacha maneno
- Makosa ya tafsiri sisi

Athari; Madharaau dosari inayotokana na makosa yafanywayo na wanafunzi kwa matokeo yao. Kulingana na utafiti huu, mtafiti alitumia istilahi athari kulejelea matokeo ya wanafunzi.

Matokeo. Mtafiti anatumia neno matokeo kumaanisha alama kutokana na mitihani iliyofanywa na wanafunzi wa Kiswahili.

Ufasaha: Umilisi wa kutumia lugha husika bila makosa au dosari yoyote katika sentensi na kwa mjibu wa utafiti huu ufasaha ni wa lugha ya Kiswahili. Uchanganuzi makosa. Ni uchunguzi wa chazo cha makosa ya aina mbalimbali; Hufafanua makosa ya mwanafunzi wa luha ya pili.

Nadharia ya uchanganuzi makosa; Nadharia hii (NUM) ilianzishwa na Corder (1969), na kuendelezwa na Etherton (1977), Narrish (1983) na huchunguza makosa kwa kuyatambua, kuyaainisha na kufafanua chazo cha makosa hayo: Katika utafiti huu, nadharia ya uchanganuzi makosa ni makubaliano yaliyopendekezwa kuchambua chanzo cha makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi.

Matokeo mabaya. Kwake Eke (1986) matokeo mabaya ni alama za hadhi ya chini na zisizowaridhisha wanafunzi na wadau wengine. Katika utafiti huu, dhana hii ilitumiwa kumaanisha upataji wa alama chache (chini ya alama hamsini) katika mitihani ya Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Uganda.

MBINU ZA UTAFITI

Utangulizi

Sura hii imeelezea aina ya utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli ya utafiti, mbinu za ukusanyaji wa data na mbinu zilizotumika katika uchanganuzi wa data.

Aina ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa ni wa nyanjani. Ulichunguza athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Metropolitan Magharibi mwa Uganda

Eneo la Utafiti

Ngure, (2011:198), anaeleza kwamba inabidi kuamua ni wapi utakusanya data utakayohitaji. Kwa hivyo, utafiti huu ulikuwa utafiti wa nyanjani na ulikusanywa Chuoni Metropolitan Magharibi mwa nchi ya Uganda Jijini Mbarara. Mtafiti alichagua Chuo hicho kwa sababu kinapatikana sehemu ya Magharibi mwa Uganda na chenye historia ya kujifundisha Kiswahili kwa muda mrefu kuliko vyuo vingine katika sehemu hiyo.

Kundi Lengwa

Walliman (2011), anafafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika utafiti (vinavyuotafitiwa), yaani, watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa ujumla, kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Katika utafiti huu, kundi lengwa ni wanafunzi wanaojufunza Kiswahili Chuoni Metropolitan pamoja na wahadhiri wao (wataalam wa lugha ya Kiswahili).

Sampuli ya Utafiti

Babbie, E (1999), anadai kwamba, sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutia nayo katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Sigh (2007),

anadai kuwa, usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Kothari, (2008) amependekeza kuwa, sampuli isiwe kubwa au dogo bali iwe ya kati. Mtafiti aliteua sampuli ya utafiti wake kulingana na sifa kuwa na wana uwezo wa kutoa data sahihi zinazotakiwa kulingana na malengo ya utafiti huu; yaani, waliokuwa na uwezo wa kutoa habari faafu zilizojibu kikamilifu maswali ya utafiti. Kwa hivyo, sampuli ya mtafiti ilikuwa ni wanafunzi mia moja na wa tano na wahadhiri wawili wa Kiswahili Chuoni Metropolitan Jijini Mbarara Magharibi mwa Uganda. Mtafiti alichagua wanafunzi mia moja na tano huku akichagua wanafunzi therathini na wa tano katika mwaka wa kwanza, wanafunzi therathini katika mwaka wa pili na wanafunzi arobaine katika mwaka wa tatu; mtafiti alitumia wanafunzi mia moja na watano ili kuwapatia nafasi yakutoa maoni yao bila uchaguzi. Vile vile, mtafiti aliwahasisha wahadhiri wawili kushughulikia utafiti huu na kueleza maoni yao kuhusu athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi Chuoni chao. Mtafiti alitumia wadhiri wawili kwa sababu ndio waliopatikana Chuoni wakati wa kukusanya data.

Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu ziliyotumiwa katika ukusanyaji wa data zilikuwa ni hojaji na uchunguzi shiriki kwa sababu ndizo zilizoweza kutumia malengo ya utafiti huu. Mtafiti alitumia hojaji kwa wanafunzi na wahadhiri kwa kuwapatia nakala wasailiwa na baadaye kurejelea maoni yao. Hojaji ziliandaliwa kulingana na madhumuni ya utafiti huu. Mtafiti alitumia hojaji ili kupata data ya msingi na kuwapatia uhuru wa wahojiwa ili watowe maoni yao. Pia mtafiti alitumia uchunguzi shiriki kwa wanafunzi wa Kiswahili kwa kutumia zoezi imla. Mtafiti alitumia mbinu ya uchunguzi shiriki ili kupata umilisi wa msingi wa wanafunzi wa Kiswahili. Data iliyopatwa ilirekodiwa nakufasiriwa kwa kutumia jedwali.

Uchanganuzi wa Data

Kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya uchanganuzi makosa; mtafiti alichanganua data yake kwa kutumia mbinu ya kithamano.

UCHANGANUZI WA DATA

Utangulizi

Sehemu hii imebainisha aina za makosa ya kisarufina jinsi yalivyochanganuliwa. Mtafiti aliongozwa na vigezo vya aina mbili ambavyo ni madhumuni ya utafiti na mihimili ya nadharia. Baada ya kuchunguza makosa katika uandishi wa insha. Kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wa pili, mtafiti alichunguza athari za lugha ya kwanza katika mazungumzo miongoni mwa wanafunzi na matumizi ya lugha ya Kiswahili ili kupima ufasaha wao. Baada ya kukusanya insha wahojiwa walipewa kazi za imla ili waiandike na kuisoma. Hatimaye mtafiti alichambua makosa yao ya kimaandishi na kimatamshi yaliyofanywa na wanafunzi walipokuwa wakizungumza na kujibu zoezi walilopewa katika insha naimla namwishoni kuchanganua kazi za wanafunzi. Kila mwaka ulipewa mada ya insha moja kati ya mada zilizopo katika viambatisho.

Makosa ya Kisarufi Yaliyobainika kwa Wanafunzi

Mtafiti nyanjani aliwalenga wanafunzi katika maandishi ya insha na Makosa yaliyobainika baada ya kuwasaili ni yale yanayotokana na undaji wa taratibu na kanuni za kisarufi. Makosa hayo ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi katika inshazaoza Kiswahili yaliwekwa katika makundi mbalimbali.

Makundi hayo ni; makosa ya mpangilio wa vipashio katika sentensi, makosa ya upatanishi wa kisarufi, makosa ya kuongeza vitamkwa, makosa ya matumizi ya maneno ambayo si mwafaka, makosa ya kimatamshi, makosa ya hijai , kutenganisha maneno, matumizi mabaya ya vivumishi, herufi kuachwa katika neno, utumiaji wa herufi zisizofaa katika neno, kuongeza herufi kwenye neno, matumizi ya kirejeshi “ amba”, sentensi tata, matumizi ya kiambishi tamati “ni”, kiunganisha ‘katika’, matumizi ya kivumishi --enye, kunyambua nomino badala ya kunyambua vitenzi, kuchanganya ngeli, kurudia rudia maneno katika sentensi, matumizi ya “jinsi” na ‘namna’, matumizi ya ‘katika’ na ‘kwenye’, makosa katika uandishi wa semi, kutotumia ritifaa au

kutoakifisha vizuri ,athari za kiingereza na lugha mama, makosa ya muundo wa sentensi.

Makosa ya kisarufi yaliainishwa katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na.2 Makosaya Mpangilio wa Vipashio katika Sentensi

Kosa	Usahihi
Kiwanda mjini kitajengwa	Kiwanda kitajengwa mjini
Atakuja mtoto yule shuleni	Mtoto yule atakuja shuleni
Ile meza ni nzuri sana	Meza ile ni nzuri sana
Mama mtoto atazaa	Mama atajifungua mtoto
Lia usiku uta kila	Utalia kila siku
Tabia mzuri Brenda ana	Brenda ana tabia nzuri
Lala kitanda yeye	Yeye alilala kitandani
Kesho walikelele piga	Keshoye walipiga kelele

Jedwali lapililinaonyesha kwamba, sentensi za Kiswahili kawaida huanza na nomino ya mtenda, mtendewa au mtendewa, mtafiti aligundua kuwa wanafunzi mara nyingi hawakufuata kanuni hii. Kwa hivyo ni muhimu kwa wanafunzi kujizoesha kusoma vitabu vya Kiswahili wakizingatia mpangilio wa maneno ya Kiswahilikatika sentensi.

Jedwali Na.3Makosa ya Upatanishi wa Kisarufi

Kosa	Usahihi
Nimepoteza kalamu wangu	Nimepoteza kalamu yangu
Meza wangu ameanguka	Meza yangu imeanguka
Mtoto yangu kimekuja	Mtoto wangu amekuja
Kijiko wangu ni mkubwa	Kijiko changu ni kikubwa
Maji wangu mdogo	Maji yangu kidogo
Kitanda wake simzuri	Kitanda chake si kizuri
Wowote ni wanafunzi	Wao wote ni wanafunzi

Tulibeba mzigo letu	Tulibeba mizigo yetu
Mgonjwa kilienda	Mgonjwa alienda
Chakula yote pika	Pika chakula chote

Katika jedwali la 3, mtafiti aligundua kuwa makosa ya aina hii hutokea wanafunzi wanapochanganya upatanishi wa kisarufi. Wanafunzi hawaelewi vivumishi na vimilikishi vya kila ngeli. Ndiyo sababu makosa kama hayo yanajitokeza. Wanafunzi ni muhimu wajifunze vivumishi, kimilikishi na viambishi vya kila ngeli ili waelewe matumizi yake katika sentensi.

Jedwali Na.4 Makosa ya Kuongeza Vitamkwa

Kosa	Usahihi
Ninasomeanga shule hii	Ninasomea shule hii
Mtoto geni amefikako	Mtoto mgeni amefika
Nipeko chakula	Nipe chakula
Aliwaambiao kuleta vitabu	Aliwaambia walete vitabu
Twambieo ukweli	Twambie ukweli
Msomeeko kitabu	Msomee kitabu
Alimwitako mama	Alimwita mama
Lalapo hapa	Lala hapa
Baba alikuweko shuleni	Baba alikuwa shuleni
Kulako kidogo	Kula kidogo

Katika jedwali la nne, mtafiti alitambuwa kuwa baadhi ya wanafunzi huongeza vitamkwa mahali pasipotakiwa na hivyo huvuruga utaratibu wa kujenga maneno na uandishi wa insha. Katika sentensi ya kwanza mwanafunzi aliongeza kitamkwa “nga” katika neno somea. Sentensi ya pili wanafunzi waliongea “ko” katika neno fika. Sentensi ya tatu kwa upande wa makosa mwanafunzi aliongeza “ko” kwenye neno nipe. Na sentensi ya mwisho aliongeza “o” katika neno ambia. Sababu ya kufanya hivyo ni uzoefu wa kutumia na kusikiliza wazungumzaji wa lugha ya kwanza. Ni muhimu sana wanafunzi kusikiliza habari na vipindi vinginevyo vya lugha ya Kiswahili redioni ili

waweze kuwa na matamshi mazuri ya maneno ambayo yatawasaidia kuandika Kiswahili sanifu.

Jedwali Na.5 Makosa yaMatumizi ya Maneno ambayo si Mwafaka

Kosa	Usahihi
Kondoo amenenepa	Kondoo amenona
Chunga mazingara	Tunza mazingira
Barabara inakwenda mjini	Barabara inaelekea mjini
Tutakuwa wazuri	Tutakuwa wanafunzi wazuri
Walipeza zao	Walipoteza pesa zao
Anapenda sisi	Anatupenda sisi
Mbuzi hupenda nyasi	Mbuzi hupenda kula nyasi
Mtoto anafungua macho	Mtoto anaona
Kosa hilo lisuluhisho	Kosa hilo lirekebishe

Katika jedwali la tano, mtafiti alivumbua kuwa makosa ya kuacha neno ilitokea pale wanafunzi wanapotumia msamiati usiyo sahihi kwa sababu ya kutojua neno rasmi au kwa sababu ya kuandika kwa haraka wanaruka hilo neno kabisa. Wanafunzi wanatakiwa kuwa makini wakati wa kuandika mitihani ili waweze kuepukana na urukaji wa maneno

Jedwali Na. 6 Makosa ya Kimatamshi

Kosa	Usahihi
Mimi hura ugari	Mimi hula ugali
Huyu ni lafiki yangu	Huyu ni rafiki yangu
Tayarisa samba	Tayarisha shamba
Unasani ni mimi	Una dhani ni mimi
Kuhairisha	Kuahirisha
Kutekeresa	Kutekeleza

Kabuli	Kaburi
Terekamu	Teremka
Suhilusho	Suluhisho
Balidisha	Badilisha
Rekebisa	Rekebisho

Haya ni makosa ya kimatamshi ambayo mtafiti aligundua miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Metropolitan Magharibi mwa Uganda. Makosa haya yalitokana na athari ya lugha mama. Mtafiti aligundua kuwa mara nyingi makosa ya kimatamshi yanaathiri maandishi wanafunzi huandika maneno kama wanavyoyatamka. Wanafunzi hubadilisha sauti katika neno na kuishia kwa kuandika neno ambalo si sahihi. Isitoshe mtafiti aligundua kuwa makosa haya ya kimatamshi hutokea pale wanafunzi wanaposhindwa kutamka baadhi ya sauti za Kiswahili ambazo hazipatikani kwenye lugha mama. Kwa mfano kutamka “r” badala ya “l” kama jedwali linavyoonesha hapo juu. Wanafunzi wanatakiwa kufanya mazoezi ya kutamka sauti ambazo hazipatikani kwenye lugha zao za kwaza ili waweze kuboresha matamshi na pia maandishi ya maneno ya Kiswahili.

Jedwali Na.7 Makosa ya Hijai

Kosa	Usahihi
Kwa sababu	kwa sababu
Kwahiyo	kwa hivyo
Inamana	ina maana
Marakwamara	mara kwa mara
Vile vile	Vile vile
Kamavile	kama vile
Amakweli	ama kweli
Na kadhalika	na kadhalika

Kulingana na jedwali la saba, wanafunzi waliunganisha maneno ambayo yanastahili kuwa maneno mawili au matatu na kuyaandika kama neno moja. Hili pia ni kosa la kisarufi kwa sababu wanafunzi hawajazingatia tahajia ya neno kama ilivyo. Wanafuzi wakifanya hivi huishia kwa kuwa na maneno ambayo haina maana katika sentensi za lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wajizoeshe kusoma vitabu vya Kiswahili wazingatia tahajia ya maneno mbalimbali.

Jedwali Na. 8 Kutenganisha Maneno

Kosa	Usahihi
Ali kuwa	Alikuwa
Wali enda	Walienda
Vilivyo vutia	Vilivyovutia
Tulipo wasili	Tulipowasili
Wana cheza	Wanacheza
Yo yote	Yoyote
Wali kimbia	Walikimbia
Pilika pilika	Pilikapilika
Po pote	Popote

Kisarufi, wanafunzi walitenganisha maneno ambayo katika lugha ya Kiswahili yanastahili kuwa neno moja na kuyaandika kama maneno mawili. Ujifuzaji wa lugha ya pili hutegemea pia uandishi sahihi wa maneno katika lugha husika. Ni muhimu pia mwalimu kufundisha wanafunzi umuhimu wa kusoma vitabu mbali mbali vya Kiswahili kwa kuzingatia maandishi ya maneno ya Kiswahili.

Jedwali Na. 9 Matumizi Mabaya ya Vivumishi

Kosa	Usahihi
Mwanafunzi msafi	Mwanafunzi safi
Mtoto mbora	Mtoto bora

Alileta machungwa makumi	Alileta machungwa kumi
Wanafunzi kumi na wasabi	Wanafunzi kumi na saba
Wanajeshi wa malidadi	Wanajeshi maridadi
Vitabu visita	Vitabu sita
Vifaa viharisi	Vifaa halisi
Mwimbaji mbora	Mwimbaji bora
Mvuvi mhodari	Mvuvi hodari

Kulingana na jedwalihili kuna vivumishi ambavyo havibadiliki yaani havichukui viambishi ngeli. Katika matumizi yake hubaki hivyo katika ngeli zote nakatika hali ya umoja na wingi. Vivumishi kama safi kwenye sentensi ya kwanza hakichukui kiambishi ngeli kwa hali yoyote. Kwa hivyo, yafaa wanafunzi wasome vitabu vya Kiswahili wakizingatia sentensi sahihi katika umoja na wingi. Kila mara wafanye mazoezi ya vivumishi hivi ili wavielewe barabara. Pia waelewe kuzingatia ngeli zote wakati wa kuandika sentensi.

Jedwali Na. 10 Herufi kuachwa katika Neno

Kosa	Usahihi
Siku hio	Siku hiyo
Kueka vitu kichani	Kuweka vitu kichwani
Alisuka chini	Alishuka chini
Awezi kutembea	Hawezi kutembea
Awezi kusoma vitabu	Hawezi kusoma vitabu
Asubui	Asubuhi
Badae	Baadaye
Kusima	Kusimama
Samba langu	Shamba langu
Mandishi	Maandishi

Katika jedwali la 10hapo juu, wanafunzi walikuwa na makosa ya kuacha herufi katika neno. Jambo hili lililetea mwanafunzi kuwa na maneno ambayo hayaeleweki kama yanavyoonyeshwa hapo juu kwa upande wa makosa. Vyanzo vya makosa hayo vyaweza kuwa kuandika kwa haraka au kutopitia kwenye kazi baada ya kuandika ili kukosowa makosa hayo. Ni jambo la muhimu wanafunzi kupitia kwenye kazi mara mbili au zaidi ili kukosoa makosa ya kitahajia na muundo mbaya wa sentensi.

Jedwali Na. 11 Utumiaji wa Herufi zisizofaa katika Neno

Kosa	Usahihi
Misichana	Msichana
Muti	Mti
Dakitari	Daktari
Dalasa	Darasa
Fuaua	Fuata
Mumeya	Mmea
Mulima	Mlima
Vinamaasi	Vinamasi
Maporoomoko	Maporomoko

Kulingana najedwali hili wanafunzi walikuwa na makosa ya kuweka herufi isiyofaa katika neno. Jambo hilo huletea insha kutokuwa na maana iliyokusudiwa kama jedwali linavyoonyesha hapo juu. Utumiaji wa herufi zisizofaa katika neno hutatuliwa wanafunzi wakuandika maneno haya kwa madaftari yao na kueleza maana yake.

Jedwali Na. 12 Kuongeza Herufi kwenye Neno

Kosa	Usahihi
Atatembeya	Atatembea
Chukuwa	Chukua
inje ya darasa	Nje ya darasa
inchini Uganda	Nchini Uganda

Katika jedwali hili, mwanafunzi alifanya kosa kwa kuweka (y) kati ya irabu (e) na (a) na kuwa na neno “tembeya” badala ya kuandika “tembea” ambalo ndiyo neno sahihi. Makosa ya aina hii yaweza kuepukwa wanafunzi wakiandikiana barua na kuzisoma Aidha wasome vitabu vya Kiswahili kila mara.

Jedwali Na. 13 Matumizi ya Kirejeshi “Amba”

Kosa	Usahihi
Mwanafunzi ambayo alikuja hapa	Mwanafunzi ambaye alikuja hapa
Kitabu ambacho kililetwa jana	Kitabu kilicholetwa jana
Mtoto ambayo alikufa	Mtoto ambaye alikufa
Jina ambayo yalisoma	Jina ambalo alisoma
Mwizi ambao alishikwa	Mwizi ambaye alioshikwa
Chakula ambaye kitapikwa	Chakula ambacho kitapikwa
Mti ambaye ulikatwa	Mti ambao ulikatwa

Kiambishi kirejeshi amba hutumiwa kurejelea jina lililotajwa. Kiambishi hiki hufuata utaratibu wa ngeli. Wanafunzi wengi walikosa katika kurudia kirejeshi hicho. Sentensi katika jedwali hili kwa upande wa kosa ziliandikwa na wanafunzi. Matumizi ya kirejeshiamba huweza kukomeshwa kwa wanafunzi kutumiatena amba kama kirejeshi changeli hiyo kwenyekitenzi kinachofuata. Wanafunzi wafunzwe na kusoma matumizi sahihi ya kirejeshi amba katika ngeli zote. Wanafunzi aidha wafanye mazoezi mengi katika vipindi vya darasani,

Jedwali Na. 14 Sentensi Tata

Kosa	Usahihi
Walivua nguo	Walifua nguo
Alikua akicheza na mamaye	Alikuwa akicheza na mamaye
Inchini kua watu wengi	Nchini kuna watu wengi
Mambo alienda gobo	Mambo yalienda kombo
Shombo chilizama	Chombo kilizama

Avya yake ni mbaya	Afya yake ni mbaya
Shanduku lililetwa mjini	Sanduku lililetwa mjini
Walimchika mkono	Walimshika mkono

Kulingana na jedwali hili hapo juu wanafunzi walitumia maneno yanayotatanisha. Waliandika neno “alikua” badala ya “alikuwa”, “inchini” badala ya “nchini”, ‘gobo’ badala ya kuandika “kombo”, “shombo” badala ya neno “chombo” na mwishoni katika mfano wa mwisho, aliandika neno “avya” Makosa hayo yote ya maneno yanayotatanisha huletea tungo kupoteza maana. Makosa haya huweza kukoma kwakuwashauri wanafunzi wafanye mazoezi mengi ya matamshi kuhusu maneno yanayotatanisha napia wayatumie kutunga sentensi sahihi na baadaye wazisahihishe wenyewe.

Matumizi ya Kiambishi Tamati ‘ni’ pamoja na Kiunganishi ‘katika’

Kiambishi tamati “ni” kinawekwa mwishoni mwa neno. Yaani kikitanguliwa na jina la ngeli yoyote. Kwa mfano Ndani ya kitu, Mahali fulani, Kueleza jambo au wahusika zaidi ya mmoja.

i) Kuonyesha Wingi waWahusika

Kiambishi “ni” kikitumiwa mwishoni mwa kitenzi huonyesha wingi wa wahusika. Kwa mfano ukiwa unamshukuru tu mmoja unasema asante lakini wakati wa kuwashukuru au kuamrisha watu wengi utasema asanteni.

Jedwali Na. 15 Matumizi ya Kiambishi Tamati “ni”

Umoja	Wingi	makosa ya wanafinzi
Ingia	Ingieni	Ingiani
Soma	Someni	Somani
Panda	Pandeni	Pandiani
Lia	Lieni	Liani
Imba	Imbeni	Imbani

Fungua	Fungueni	Fungani
Piga	Pigeni	Pigana
Fungua	Fagueni	Funguani
Jibu	Jibuni	
Jaribu	Jaribuni	
Inama	Inameni	Inamani
Tembea	Tembeeni	tembeani

Jedwali hili linaonyesha matumizi ya ‘ni’ kuonyesha wingi wahusika. Kiambishi “ni” kikitumiwa mwishoni mwa kitezi huonyesha wingi wa wahusika. Kwa mfano ukiwa unamshukuru mtu mmoja unasema asante lakini wakati wa kuwashukuru au kuamrisha watu wengi utasema asanteni. Mtafiti aligundua kwamba, wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan walishidwa kutumia kiambishi tamati “-ni” kwa kuonyesha wingi wa wahusika kilichoathiri matumizi ya kiambishi tamati katika maandishi yao. Kwao wengi, waliingiza silabi ni kwa mwisio wa kila kitenzi bila kutambua athari ya kiambishi tamati kwa kwa kiishio cha kitenzi.

ii) Kiunganisha ‘katika’ hutumika kuonyesha ndani ya hali fulani.

Mifano katika sentensi ni:

Mwalimu mkuu yuko katika ofisi (ndani ya ofisi)

Mama yumo katika chumba (ndani ya chumba)

Weka vitaku katika nyumba (ndaniya nyumba)

Jedwali Na. 16 Kiunganisha ‘katika’

Kosa	Usahihi
Ninasomea katika Chuo Kikuu cha Metropolitan.	Ninasomea Chuo Kikuu cha Metropolitan
Mama yuko katika chumbani chake	Mama yumo chumbani mwake
Tulilala katika kitandani	Yulilala kitandani
Nyoka ameingia katika Chuo cha walimu Kabale	Nyoka ameingia Chuo cha walimu Kabale
Mbuzi atalala katika chumbani	Mbuzi atalala chumbani
Nita kaa katika kiti	Nitakakaa kitini
Watatembea katika injiani	Watatembea njiani
Atambeba katika mimkononi	Atambeba mikononi

Jedwali hili linaonyesha namna wanafunzi walivyofanya makosa kwa kutumia kiamabishi “katika” na ‘ni’ katika sentensi moja. Viambishi hivi viwili havitumiki kwenye sentensi moja kwa hali yoyote. Matumizi ya kiambishi tamati “ni” na kiunganishi “katika” ni heri kukumbuka ya kwamba kiishio “ni” na kiunganishi “katika” havitumiki pamoja kamwe katika sentensi. Hivyo basi yafaa wanafunzi wafanye mazoezi mengi ya aina hii na pia watungiwe sentensi zilizovurugwa ili wazisahihishe

Jedwali Na. 17 Matumizi ya Kivumishi --enye

Kosa	Usahihi
Mtoto mwenye anakuja	Mtoto anayekuja
Vyombo vyenye kuchafuka	Vyombo vilivyochafuka
Matunda yenye yameoza	Matunda yaliyooza
Gali lenye linasafishwa	Gari linalosafishwa

“-Enye- “ni kivumishi cha pekee ambacho huonyesha umilikaji au hali ya kuhodhi kitu, mtuau jambo. Wanafunzi wengi walikosea sana katika matumizi ya neno hili walipokuwa wakiandika insha. Nimuhimu wanafunzi waelewe ya kuwa ni kosa kubwa kutumia kivumishi “-enye” pamoja na kitenzi. Kivumishi –enye- hakifuatwi kamwe na

kitenzi bali hufuatwa na jina. Hivyo basi, ni muhimu wanafunzi kusoma vitabu vya sarufi ili waweze kuwa na matumizi ya kivumishi enye bababara.

Jedwali Na. 18 Kunyambua Nomino Badala ya Kunyambua Vitenzi

Kosa	Usahihi
Nilikimya	Nilikaa kimya
Kugonjeka	Kuwa mgonjwa
Kutia tamatisha	Kutia tamati
Kuisha	Kuishiliza

Jedwali hili linaonyesha makosa ambayo wanafunzi walifanya wakati kuandika insha. Baadhiya wanafunzi walifanya makosa mengi sana ya kisarufi ya kunyambua nomino badala yakunyambua vitenzi. Ni muhimu wanafunzi kuelewe ya kwamba majina asilia hayanyambuliwi wala hayanyambuliki. Ni vitenzi tu ambavyo hunyambuliwa.

Jidwali Na. 19 Kuchanganya Ngeli

Kosa	Usahihi
Vitabu zetu zimepotea	Vitabu vyetu vimepotea
Gari yangu ni mazuri	Gari langu ni zuri
Mwalimu yule kilikuwa mzuri	Mwalimu yule alikuwa mzuri
Jitu yale linatisha	Jitu lile linatisha
Masikini mirefu	Maskini mrefu
Kijiko mkubwa	Kijiko kikubwa
Chumba lidogo	Chumba kidogo
Mwalimu kizuri	Mwalimu mzuri
Wazee lile	Mzee yule

Jedwali hili linaonyesha namna wanafunzi walivyofanya makosa kwa kuchanganya viwakilishi, vivumishi na viambishi vya ngeli. Wanafunzi wengi walichanganya ngeli mbalimbali katika sentensi zao. Hili ni kosa la kisarufi linalovuruga maana na muundo

wa sentensi. Kosa hilo pia huadhibiwa na kupoteza alama za mwanafunzi. Wanafunzi wanashahuriwa kusoma na kuelewa ngeli na viambishi vyake pamoja na viwakilishi vyake ili kuimudu lugha. Wallah Bin Wallah alisema “Asiye jua ngeli hajui lugha ya Kiswahili”. Wanafunzi wasome vitabu vinavyoelezea zaidi ngeli na wafanye mazoezi mengi kuhusu ngeli za majina. Walimu wafundishe ngeli kwa undani kwa sababu ngeli ndizo sekondari wa lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na.20 Kurudia Rudia Maneno katika Sentensi

Kosa	Usahihi
Nilimkuta mwalimumwalimu akilia sana	Nilimkuta mwalimu akilia sana
Wanafunzi walienda enda shuleni	Wanafunzi walienda shuleni
Mzazi mzazi alijibu swali	Mzazi alijibu swali
Wakunga wote wote watakimbia	Wakunga wote watakimbia
Wakajibu jibu maswali wakaendelea	walijibu maswali na wakaendelea
Walijaribu jaribu kuandika	Walijaribu kuandika

Jedwali hili linaonyesha sentensi ambazo zina maneneo yaliyo rudiwa rudiwa. Wanafunzi wengi walifanya makosa ya kurudia rudia neno moja katika sentensi ili ili kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Chazo cha kufanya makosa hayo kinaweza kuwa kuharakisha kwa wanafunzi wakati wa kuandika insha na kutorudia kusoma katika kazi hiyo baadaya kuandika. Kwa hivyo wanafunzi wapitie kweye kazi yao mara tatu ili waweze kuwa na kazi isiyo na makosaya kisarufi.

Jedwali Na. 22 Matumizi ya “jinsi” na ‘namna’

Kosa	Sahihi
Jinsi alicheza	Jinsi alivyocheza
Namna atasoma	Namna atakavyosoma
Jinsi atamwona	Jinsi atakavyomwona
Namna alisema	Namna alivyosema

Jinsi alilala

Jinsi alivyolala

Wanafunzi walitumia Jinsi alicheza badala ya jinsi alivyocheza, namna atasoma, badala ya namna atakavyosoma, jinsi atamwona badala ya jinsi atakavyosoma, namna alisema badala ya namna alivyo sema, jinsi alila badala ya Jinsi alivyolala na kwa hivyo, makosa haya yalijitokeza katika mitihani na kusababisha matokeo mabaya. Yaani; Jedwali hili lilionyesha matumizi mabaya ya neno ‘jinsi’ na ‘namna’ na jinsi yanavyoweza kutumiwa vizuri ili kuepuka makosa ya kisarufi. Jinsi, namna nakadri nimajina ilhali kama, ndiyo na vile ni vielezi. Maneno haya yanapotumiwa wakati wowote katika kila sentensi na kufuwa na kitenzi ama kitenzi kisaidizi ni sharti “vyo” itumike kama ilivyoonyeshwa hapo juu kwa upande wa usahihi.

Jedwali Na. 22 Matumizi ya ‘Katika’ na ‘Kwenye’

Kosa	Usahihi
Mtoto ameingia kwenye nyumba	Mtoto ameingia katika nyumba
Mwalimu alisimama kwenye nyumba	Mwalimu alisimama katika nyumba

Jedwali hili linaonyesha matumizi mabaya ya neno “katika” na “kwenye”. Pia linaonyesha matumizi mazuri ya maneno hayo kwa upande wa usahihi. Neno ‘katika’ hutumika kumaanisha ndani ya. “Kwenye” hutumika kumanisha “kuliko na”. Kwa hivyo wanafunzi wanasitahili kuainisha tofauti iliopo kati ya maneno haya mawili na matumizi ya maneno yenyewe katika sentensi za lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na. 23 Makosa katika Uandishi wa Semi

Kosa	Usahihi
Chungu muzima	chungu nzima
Pika ndoo teke	Piga ndoo teke
Pika mswaki	piga mswaki
Tia bidii	tia adabu
Kujitahidi kisabuni	kujikaza kisabuni
Kuhaga dunia	kuaga dunia

Chika tama	shika tama
Piga goti	piga magoti

Wanafunzi wengi walikosea katika semi. Yaani misemo na methali. Haya ni mapokezi kutoka kwa wasisi au waanzilishi wake na hivyo haistahili kubadilishwa kwa namna yoyote ile. Nisharti misemo na methali ibaki hivyo hivyo bila kubaadilisha hata neno moja. Ni makosa kwa mwanafunzi kubadilisha au kuondoa neno moja na kutumia kisawe chake neno katika msemu na methali. Wanafunzi wanashauriwa kusoma methali na misemo mara kwa mara ili wazielewe vyema pamoja na matumizi yake sahihi.

Jedwali Na. 24 Kutotumia Ritifaa au Kutoakifisha vizuri

Kosa	Sahihi
Ngombe	ng'ombe
Nongona	nong'ona
Ngoa	ng'oa
Nyang 'ganya	nyang'anya
mgao	mg'ao
nga'n'gania	ng'ang'ania
ng'amia	ngamia
ngam'bo	ng'ambo

Katika jedwali la ishirini na tano, wanafunzi walitumia ratifaa lakini ratifaa zao ziliwekwa pahali pasipo faa. Suluhisho la kosa la aina nikwamba wanafunzi wasome makala na vitabu vya Kiswahili wakizingatia tahajia sahihi ya maneno yanayotumia ratifaa.

Jedwali Na. 25 Athari za Kiingereza na Lugha mama

Kosa	Usahihi
Nitawambia weije nyumbani	Nitawambia waje nyumbani
Twende field kulima	Twende shambani kulima

Stand twende sokono	Simama twende sokoni
Beba food twende shuleni	Beba chakula twende shuleni
Ente yangu ni ngonjwa	N'gombe wangu ni mgonjwa

Katika jadwali la hapo juu linaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi wanaathiriwa na lugha nyinginezo kama vile Kiingereza na lugha mama. Katika Sentensi ya kwanza kuna neno “waije” ambalo linatokana na lugha ya mama ya mwanafunzi na sentensi ya pili kuna neno la Kiingereza “field”. Badala ya kutumia neno shambani ambalo ndiyo sahihi wanafunzi walitumia neno ‘field’ la kiingereza.

Jedwali Na. 26 Makosa ya Muundo wa Sentensi

Kosa	Usahihi
Tumeona dunia katika mengi	Duniani kuna mengi
Alileta chakula badala ya kazi	Alileta chakula baada ya kazi
Usilete kuku na mchele	Usilete kuku kwa wali
Watoto yangu ni vijana mbili	Watoto wangu ni wavulana wawili
Meza yule amechafuka sana	Meza ile imechafuka sana
Kitabu wangu vina uchafu	Kitabu changu kina uchafu
Tulienda kumtafuta hatukukiona	Tulienda kumtafuta hatukumuona
Huyu ni jani la mti	Hili ni jani la mti
Nanasi zote alioza	Nanasi zote zilioza
Chakula yange ni kitamu	Chakula changu ni tamu sana

Haya ni Makosa yaliyopatikana katika insha walizopewa wanafunzi. Makosa haya yalidhihirisha kuwa wanafunzi wengi walipata alama za chini ya ishirini kwenye insha zao. Wengi wao hujua kuandika insha kwa Kiswahili kianachoeleweka. Mtafiti alitambua makosa yakisarufi hutokeapale wanafunzi wanapozungumza au kuandika huku wakiunda sentensi ambazo hazizingatii utaratibu aumpangilio wa manenoyanayokubaliwa katika lugha ya Kiswahili sanifu. Jedwali la 27 linafafanua zaidi makosa hayo kwa upande wa kosa na usahihi wake kwa upande wa usahihi.

Jedwali Na. 27 Matumizi ya Makosa ya Msamiati katika Kutafsiri Sentensi.

Sentensi Katika Kingereza	Makosa Yalioandikwa na Wanafunzi katika utafsiri	Sentensi Sahihi
This book is very expensive	Kitabu hiki ni cha bei ya juu.	Kitabu hiki ni cha bei ya ghali
That table is very good	Meza zile ni nzuri nyoo	Meza ile ni nzuri sana
My daughter has been beaten	Binti zangu amepigwa	Binti yangu amepigwa
That line is short.	Mushorongo huyo ni mfupi	Mshororo huo ni mfupi

Katika jadwali la hapo juu linaonesha makosa yafanywayo na wanafunzi katika kutafsiri kazi kutoka lugha ya kingereza kwa Kiswahili. Wanafunzi walifanya makosa ya kimsamiati walipokuwa walitafsiri sentensi katika kazi zao. Kwa hivyo makosa hayo yaliathiri kisarufi kilichosababisha matokeo mabaya katika mitihani yao.

Katika jadwali la hapo juu linaonesha makosa yafanywayo na wanafunzi katika kutafsiri kazi kutoka lugha ya kingereza kwa Kiswahili. Wanafunzi walifanya makosa ya kimsamiati walipokuwa walitafsiri sentensi katika kazi zao. Kwa hivyo makosa hayo yaliathiri kisarufi kilichosababisha matokeo mabaya katika mitihani yao.

Matokeo ya Utafiti

- Utafiti umegundua kwamba makosa ya kisarufi hufanywa na wanafunzi wengi Chuoni Metropolitan
- Mtafiti aligundua kuwa matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan yana athiriwa na makosa ya kisarufi yafanywayo na wanafunzi wa Kiswahili katika mitihani.

- c) Utafiti huu uligundua kuwa wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan huvishwa shahada za hadhi ya chini kinachosababishwa na matokeo mabaya katika mitihani yao yanayoathiriwa na makosa ya kisarufi.
- d) Mtafiti amebaini kwamba athari za makosa ya kisarufi yanaweza kudhihirishwa katika uwandishi wa insha na imla
- e) Kwa hivyo, mtafiti amebaini kwamba wahadhiri wangukuwa wanawapa hizo kazi za uandishi wa insha na imla na kuzisahihisha basi na makosa yangepungua au kuondoka.

Hitimisho

Utafiti huu uliegemea upande wa lugha na isimu huku uchunguzi athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Uganda. Utafiti huu ulionyesha kwamba makosa hayo ni tatizo kubwa miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Metropolitan Magharibi mwa Uganda kinachoathiri matokeo yao.

Mapendekezo ya Utafiti

Baada ya kujadili kuhusu uchanganuzi wa athari za makosa ya kisarufi katika matokeo ya wanafunzi wa Kiswahili Chuoni Metropolitan Magharibi mwa Ugandamapendekezo yafuatayo ni faafu katika suluhisho la makosa haya:

1. Ni vizuri wahadhiri wafundishe Kiswahili kwa ujumla. Watumie vitabu ambavyo vimependekazwa kulingana na silabasi ili vitumiwe kufundisha na kutegemea maswali yanayoibuka.
2. Wahadhiri wajaribu kuwapa wanafunzi mazoezi ya kuandika insha mara nyingi iwezekanavyo na waonyeshwe makosa yao.
3. Wahadhiri waongoze wanafunzi katika kuunda makundi ya kusomeana kwa sauti ili wale ambao wana shida za matamshi wasahihishwe na wenzao wenye ujuzi zaidi.

Kwa jumla, makosa haya yataepukwa iwapo wanafunzi wa Kiswahili watafanya mazoezi mengi ya kuandika makala katika lugha ya Kiswahili na kusoma vitabu vingi vya Kiswahili sanifu, kusikiliza vipindi vya Kiswahili redioni na televisheni, kusoma magazeti na majarinda ya Kiswahili, kusoma vitabu vya hadithi na vya lugha pamoja na kushirikiana na wajuzi wa lugha ya Kiswahili

MAREJELEO

Andala M. (2008). *Makosa ya kawaida katika Kiswahili*, Nairobi: Creative Print House.

Babbie, E (1999): Lhukonzo – *English dictionary*, Triple.B. Enterprises Ltd.Kasese

Broomfield, G.W (1975), *Sarufi ya Kiswahili*. Oxford; Oxford University Press

Brown.H.D. (1987), *Principles of language Learning and Teaching*, Retrieved May10, 2014 from <http://www.google.com>

Chapeton, (2008). *Cross –linguistic in fluency in writing of an Italian study*; katika Columbia applied linguistic journal no.10.

Chepkwony (2012) *uchunguzi wa matatizo ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa kipsingis. mfano Jijini Mbarara ya Bomet*. Tasnifu ya M.A (Isiyichapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta Kenya

Corder, S P. (1967). *Error analysis and interpretation*; Oxfod University press

Denis M. (1971). *Educating second language children* Oxford University press.juz la 23 nov.067 Wednesday april 2008 uk 6

Duly and Burt, (1973) *Error and strateges on child's second language learning*. In tes Quarterly, Vol.8pp129-136.

Etherton A.R. B (1977), *Error analysis, problem and procedures in English teaching*. Journal vol.32.no.1 pp 67-78

Guthrie, M. (1967) *Comparative Bantu: An Introduction to the Comparative and Per History of Bantu Language*. Amersham, England: Gregg Press Ltd

He Dan (2010) *Error analysis on English majors' writing from the perspective of inter Language; katika journal of language and literature studies*

Hymes na wengine, (1972:269-293) *On communication competence* D na J. Holmes (wa) Sociolinguistic harmonics worth Penguin

I Para I na Maina Geoffrey, (2008) *Fani ya isimu jamii kwa shule za sekondari*, Nairobi: Oxford University East Africa Ltd, Kenya

Idarus (2005): *Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili* Chuo Kikuu Dar es salaam

Jiang, N. (2004). *Semantic transfer and its implications for vocabulary teaching in a second language journal*, 88 416—432. (Open url query data cross ref google scholar

Kavogo (2007), *makosa ya kisarufi na jinsi yanavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika tarafa ya Rairieda Jijini Mbarara Bondo, miongoni mwa wanajamii ya Wajaluo.*

Kisakwah (2014) *uchanganuzi wa makosa na muundo wa sentensi katika wanafunzi wa kisiwani*

Kothari, R, C, (2008), *Research Methodology; Methods*. New Delhi New Age. International Publishing LTD Techniques.

Lucius M Thonya (1978), *missingi ya Kiswahili*, Mhenga publishing consultants Company limited

Marani, J (1994), *Athari za kikabrasi katika ujifunzaji wa Kiswahili Tasnifu ya uzamili isiyochapishwa* Chuo Kikuu cha Nairobi.

Massamba, D. P. B. (2004), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*, TUKI, Dar es salaam.

Mbaabu (1995), “*Dhima ya kamusi katika kufundisha na kujifunza Kiswahili*,” katika J.G. Kiango *Dhima ya kamusi katika kusanifisha lugha*, Dae es salaam, Tuki 47-59

Mbaabu, (1992), *sarufu ya Kiswahili*, Nairobi. Nairobi. Longman Kenya Ltd

Mbula, J.E. (2011), *Uchanganuzi wa makosa ya kifonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kikamba*; Mfano wa wilaya ya Kitui. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi

Mdee, J.S. (1986). *Kiswahili muundo na matumizi yake*, Dar es Salaam: International publishers Ltd

Mekacha R.D.K. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Mukadha wa Kiswahili*.Chuo Kikuu cha Dar es salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Mgullu, R.S. (1999), *isimujamii: Fonetiki, fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*, Longhorn publishers.

Micharia N. O Iribemwangi, P. I. na Mbatia, M. (2004). *Ukuzaji wa Kiswahili*. Nairobi Printwell Industries Ltd

Msanjila, Y.A. (2005), *Problems of writing in Kiswahili. A case study of Kigurunyembe and Morogoro sekondari school in Tanzania*. Katika Nordic journal of African studies 14 (i) 15-25. University of Dar es salaam, Tanzania

Musa, (2008), *Athari za lugha ya kigweno katika Kiswahili na jinsi kinavyoathiri matokeo Mabaya ya mitihani ya kitaifa*. Tasnifu ya uzamili (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha uislamu Mbale Uganda.

Muthu, K.F. (2005). *Uchanganuzi wa moakosa ya kisintaksia katika tafsiri za magazeti (Taifa Leo)*. Tasnifu ya PHD (Isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi

Mutunga. B.N. *Makosa ya kileksia katika insha na chanzo chake: Uchanganuzi wa shule tano za Upili Jijini Mbarara Kiambu*. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Mwangi.J.N. (2011) *Uchanganuzi wa makosa ya kimofosintaksia katika kingereza*. Mfano kutokana na wanafunzi jijini Nairobi. Tasnifu ya MA (isiyochapishwa.) Chuo Kikuu cha Nairobi

Ng'ang'a (2002), *makosa ya kisarufi katika insha za wanafunziwa darasa la saba na jinsi yanavyoshughulikiwa na walimu katika tarafa ya Ndaragwa*

Ontieri. J.O. (2010), *Uchanganuzi wa makosa katika insha za wanafunzi wa shule za upili*. Mfano wa wilaya ya Nakuru, Kenya.

Otiende, M.A (2013), *Athari za mofonolojia ya kibsuba katika matunizi ya Kiswahilikama lugha ya pili*. Tasnifu ya M.A.(UON).

Polome, E. C. (1967) *Swahili language handbook*. Washington: Centre for Applied Linguistics.

Radford, (1997) *syntactic Theory and the structure of English: A minimalist Approach* Cambridge, Cambridge University press.

Rapando, M. M. (2005) *Makosa ya kimofosintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili jijini Nairobi*. Tasnifu ya M. A (UON)

Shihanda.E.M (2000), *Tadubiri za isha mbinuna mapambo*, Kenya: longhon, Nairobi. Tembena na Norton (2008), *upataji wa lugha ya pili miongoni mwa wanafunzi wa jamii ya Wanyoli*

Taasisi ya Uchu nguzi wa Kiswahili, Dar es salaam (2004), Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la pili, Oxford University Press.

Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu Dar es salaam, (2005), makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili, Oxford University Press Publication Ltd

Tuki (2004), Kamusi ya Kiswahili sanifu. Nairobi. Oxford University press